



TAARIFA KWA:

KUTOKA:

**Wakuu wa shule,
Wasimamizi, Wazazi
Dkt. Don Coberly
Msimamizi wa Shule**

Elimu ni muhimu na kila siku ya shule iliyokosekana huwakilisha nafasi zilizopotea za kusoma. Hata hivyo, hoja msingi ya Wilaya ya Shule ya Boise ni usalama wa wanafunzi wote, ikiwa ni pamoja na wanafunzi wanaopanda basi na kutembea au kuendesha baisikeli hadi shuleni. Ikiwa wanafunzi hawawezi kusafiri kwa usalama kuelekea shuleni au ikiwa shule haziwezi kufanya kazi kwa usalama kwa sababu ya hali hatari ya hewa mjini kote, huenda shule ikafungwa.

Hatutafunga shule katika siku zenye hali ya kawaida ya majira ya baridi. Mvua ndogo ya theluji, asubuhi yenye baridi au maeneo yenye barafu sio hatari ya kutosha ili kulazimisha kufungwa kwa shule. Kukiwa na tahadhari inayofaa ikiwa ni pamoja na mavazi yanayofaa, utoaji barafu barabarani, na uendeshaji gari kwa makini, wanafunzi wanaweza kusafiri kwenda na kutoka shule kwa usalama.

Wilaya ya Shule ya Boise hushughulikia zaidi ya maili za mraba 50 za Jimbo la Ada. Tunatambua kwamba hali hutofautiana katika Wilaya nzima, hata kutoka mtaa mmoja hadi mtaa mwingine, katika visa vingine. Huenda hali zikawa za hatari sana katika eneo moja, il hali salama kabisa mahali pengine. Ikiwa wazazi wanaamini ni hatari sana kwa watoto wao kusafiri kwenda shuleni, wana chaguo la kuwaweka watoto wao nyumbani. Ikiwa shule imefungwa, itafungwa katika Wilaya nzima

Hali hatari zaidi za mara kwa mara zinazokumba shule za Boise ni:

THELUJI: Viwango vya theluji katika Mji wa Boise kwa kawaida huwa kidogo au wastani. Hata hivyo, kuna uwezekano kila mara kuwa mvua kubwa ya theluji inaweza kufanya kusafiri kwa gari au mguu kuwa hatari. Kihistoria, mvua kubwa ya theluji husababisha tu msongamano wa polepole na ajali ndogo ndogo Mjini kote. Mvua ya kawaida ya theluji haiwezi kusababisha shule kufungwa.

BARIDI: Hali hewa baridi ni kali zaidi kuliko theluji wakati wa kufanya maamuzi ya kufunga shule. Katika siku zenye baridi kali hoja yetu ni wanafunzi kutembea kuelekea shuleni. Hali hewa baridi sana pia hulemaza uwezo wetu wa kuwasha basi, ambayo husababisha kuchelewa katika njia zetu za kuwachukua wanafunzi, kuchelewa ambako ni hatari zaidi kwa waendeshaji kwa sababu ya hali hewa ya chini.

BARAFU: Barafu ndio hali ya hatari kabisa ya hali hewa wakati wa majira ya baridi. Mvua inayoganda na/au kuganda tena kwa theluji iliyoyeyuka hufanya barabara, mitaa na njia zetu za kutembea kuwa hatari sana kwa watembea kwa miguu, na magari. Hali zenye barafu huenda zikatulazimisha kufunga, hata kama inaonekana kwamba hakuna hali zingine zenye hatari zilizopo.

Je, uamuzi ufikiwa aje wa kufunga au kutofunga shule? Waakilishi kutoka mashirika ya usafiri, chombo cha hali ya hewa, wilaya ya njia kuu, mji na mashiriki ya kutekeleza sheria ya jimbo, na wasimamizi wa shule, pamoja na wasimamizi, hukagua barabara na kufuatilia maelezo usiku mzima na saa za asubuhi mapema. Tunawasiliana kwa simu mapema asubuhi ili kufikia uamuzi.

Ikiwa shule itafungwa, tutawasiliana na vituo vya hapa vya redio na runinga ili kueneza habari. Tutawatumia pia wazazi barua pepe na kuchapisha maelezo ya kufunga kwenye <http://www.boiseschools.org/emergency/index.html>